**MUHTASARI WA KIKAO CHA ASUBUHI CHA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA TAREHE 06 DESEMBA, 2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw | Joel Nkesela | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji | HWIG | Mwenyekiti |
| 2. | Bw | Athumani Mgunya | Kaimu Afisa Idara ya Kilimo Umwagiliaji | HWIG | Mjumbe |
| 3. | Bi | Dina Madeja | Mratibu wa TASAF | HWIG | Mjumbe |
| 4. | Bw | Nchanana Balele | Kaimu Mweka Hazina | HWIG | Mjumbe |
| 5. | Bw | Rashid Bundallah | Kaimu Afisa Elimu Sekondari | HWIG | Mjumbe |
| 6. | Bw | Emmanuel Ikandilo | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi | HWIG | Mjumbe |
| 7. | Bw | Nyamhanga Msabi | Kaimu Afisa Mipango | HWIG | mjumbe |
| 8. | Bw | Emmanuel Masaki | Afisa Mifugo na Uvuvi | HWIG | Mjumbe |
| 9. | Bw | Joseph Elias | Mtendaji mkuu mamlaka ya mji mdogo | HWIG | Mjumbe |
| 10. | Bw | Abdallah Mbuyu | Kaimu Mkaguzi wa Ndani | HWIG | Mjumbe |
| 11. | Bw | Joseph Mafuru | Kaimu Afisa Usafi na Mazingira | HWIG | Mjumbe |
| 12. | Bw | Juma Malendeja | Kaimu Kitengo cha TEHAMA | HWIG | Mjumbe |
| 13. | Bw | Godfrey Chezue | Kaimu Afisa Maendeleo ya jamii | HWIG | Mjumbe |
| 14. | Bw | Sebron M. Kabipe | Kaimu Afisa Elimu Msingi | HWIG | Mjumbe |
| 15. | Bw | Mohamed Mtao | Kaimu Mkuu Kitengo cha Ugavi | HWIG | Mjumbe |
| 16. | Bw. | Jahulula E. Jahulula | Kaimu Afisa Aridhi na Maliasili | HWIG | Mjumbe |
| 17. | Bw | Muhoja Lubeja | Kaimu Mganga Mkuu | HWIG | Mjumbe |
| 18. | Bw. | Anthony Marco | Afisa Biashara | HWIG | Mjumbe |
| 19. | Bw. | Dunia Ntabi | Kaimu Mwanasheria | HWIG | Mjumbe |
| 20. | Bw | Frank Alex | Kaimu Afisa Usafirishaji | HWIG | Mjumbe |
| 21. | Bw. | Erick T. Sije | Kaimu Afisa Utawala na Utumishi | HWIG | Katibu |

**SEKRETARIETI**

1. Bw. Baraka Kimoho - Mwandishi wa vikao
2. Bi. Gaudentia Iyogelo - Mwandishi wa vikao

**WKI. HWIG NA. 83/01/2021/2022 - KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kisha akakifungua kikao saa 6: 48 Mchana.

**WKI. HWIG NA. 83/02/2021/2022 - KURIDHIA AGENDA**

Kabla ya kuridhia agenda iliongezwa agenda moja. Kisha Wajumbe wakaridhia agenda zilizopendekezwa wazijadili

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 29 Novemba 2021
4. Yatokanayo na kikao cha wakuu wa Idara cha tarehe 29 Novemba 2021
5. Hoja za ukaguzi ambazo hazijajibiwa
6. Taarifa ya usafi wa mji wa Igunga

Maelezo yalitolewa kwamba POS 3 zipo offline – Watumishi hao walishaitwa ambao ni Ramadhani Chikuve,Daniel Jinge na John Salamba. POS Mashine 22 hazina uwezo wa kuchukua Mfumo wa sasa taarifa iwekwe vizuri siyo kwamba ni mbovu.

Wajumbe walihoji kuhusu 31% ufuatliaji vibali vya ujenzi kuna jitihada zozote zimefanyika. Maelezo yalitolewa kwamba majukumu mengi yanachangia hasa Miradi ya ujenzi pamoja na ukosefu wa usafiri. Wajumbe walishauri apatikane mtu mmoja awe maalum kufuatilia kibali. Aidha walishauri washirikishwe wenyeviti wa Vitongoji kudhibiti ujenzi bila kuwa na vibali vya ujenzi. Mhandisi wa ujenzi aratibu vizuri namna ya kufuatilie vibali ili mapato yapatikane.

**WKI. HWIG NA. 83/08/2021/2022- TAARIFA YA WIKI YA WAKUSANYAJI WA MAPATO KWA POS MASHINE**

Kaimu Mweka Hazina aliwasilisha taarifa hiyo.mbele ya kikao taarifa ilipokelewa na ilijadiliwa wakati wa kuwahoji wale wakusanyaji ambao POS zao zilikuwa zinasomeka zimezimwa.Wakashauri waendelee kuripoti wale ambao ni wadaiwa sugu

**WKI. HWIG NA. 83/09/2021/2022- TAARIFA YA KIKOSI KAZI (TASK FORCE) KUFUATILIA VYANZO VYA MAPATO**

Taarifa haikuandaliwa kwa maandishi, alieleza kwa kufuatilia usombaji wa kokoto kwa wakandarasi tripu zinaenda na taarifa zinazotolewa na kumwomba Mwanasheria aandae fomu ya kujaza Mkandarasi Wembere ambapo amelipa laki saba kati ya 8,700,000.

**Azimio**: Wajumbe waliazimia kwamba ufuatiliaji wa kiasi cha Tshs 8,000,000 kati ya 8,700,000 kilipwe kikao kijacho kipate taarifa.

**WKI. HWIG NA. 83/10/2021/2022- TAARIFA YA MIRADI INAYOTEKELEZWA NA HALIMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

I. **Idara ya Afya** Kaimu Mganga Mkuu aliwasilisha taarifa ya shughuli za ujenzi zinazofanyika katika zahanati nne za Jogohya umefiki 91%,Imalanguzu 92%,Ugaka 82% na Mondo 90%. Wajumbe walihoji miradi ipo nje ya muda. Aidha walieleza miradi ikamilike kikao kijacho yote iwe imekamilika.

II. **MIRADI YA COVID-19 UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA-IDARA YA ELIMU SEKONDARI.**

Kaimu Afisa Elimu Msingi aliwasilisha taarifa ya kupokelewa fedha **Tshs. 1,840,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 92 vya madarasa ambayo itawezesha kupokea wanafunzi wote ambao watafaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022.Miradi hiyo inatakiwa kukamilika kabla ya mwezi wa kwanza 2022.Wajumbe walipokea taarifa na kukubaliana kutekeleza, aidha walishauri idara ya ujenzi itoe ushirikiano wa kutosha.



CamScanner

Miradi inayotekelezwa kwa **EP4R** na fedha za COVID – 19. Alielezea kuwa shule ya sekondari **Nkinga** ujenzi umefikia **100% Shule ya Nkinga** ujenzi umefikia **80%**, **Choma** ujenzi umefikia 100%, **Choma** ujenzi umefikia **80%, Itunduru** ujenzi umefikia **100%, Buhekela** ujenzi umefikia **100%, Manonga** ujenzi umefikia **100%, Ugaka** ujenzi umefikia **100%,Kitangili** ujenzi umefikia **100%, Ziba** ujenzi umefikia **100%, Tambalale** ujenzi umefikia **100%, Mwamala** ujenzi umefikia **80%, Igunga** ujenzi umefikia **100%, Bukoko** ujenzi umefikia **90%**, **Nguvumoja** ujenzi umefikia 98%, **Mwayunge** ujenzi umefikia 80%, **Mbutu** ujenzi umefikia 100%, **Kinungu** ujenzi umefikia 80%, **Isakamaliwa** ujenzi umefikia 90%, **Simbo** ujenzi umefikia 80%, **Nkinga** ujenzi umefikia 60%, **Ziba** ujenzi umefikia 90%, **Mwashiku** ujenzi umefikia 90%, **Sungwizi** ujenzi umefikia 90% **Ngulumwa** ujenzi umefikia 80%, **Ziba** ujenzi umefikia 20%.

Afisa Mipango akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji kwenye kamati ya Ulinzi alieleza kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama iliagiza kuanzia tarehe 06 Desemba, 2021 kila mlezi wa Kata aende kwenye Kata ili kuhakikisha hadi kufikia tarehe 15 Desemba, 2021 angalau wawe wamefikia 80%. Wajumbe walihoji walezi wa Kata watafikaje , Maelezo yalitolewa kwamba utaratibu utaandaliwa Jumatano rote itaandaliwa kupeleka walezi.

### III. IDARA YA ELIMU MSINGI- UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA FEDHA ZA COVID -19

Kaimu Afisa Elimu Msingi aliwasilisha taarifa mbele ya kikao. ya fedha za COVID-19 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa vinane vyenye thamani ya **Tshs.160,000,000.00** ambapo kila darasa litaghanimu **Tshs.20,000,000.00.** Lakini pia halmashauri imepokea fedha kiasi cha Tzs. 80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambalo linajengwa Igunga shule ya Msingi .Wajumbe walipokea na kuelekeza shughuli za ujenzi zianze mapema na kuhakikisha zinakamilika kwa wakati

Aidha alielezea shughuli zilizofanyika hadi kufikia tarehe 06/12/2021 za ujenzi wa miundombinu ya Idara ya Elimu Msingi inayotekelezwa kwa fedha za mpango, **EP4R** na **COVID - 19** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika shule za Msingi **Bulyangombe** ujenzi umefikia 95%, **Itunduru** ujenzi umefikia 99% , **Chipukizi B(sanzula)** ujenzi umefikia 95%, **Kishelele** ujenzi umefikia 99%,**Igondela** ujenzi umefikia **99%, Jitegemee** ujenzi umefikia 95%, **Kalemela** ujenzi umefikia 90%, **Isenegeja** 95%,**Nguvumoja** ujenzi umefikia 90%, **Nyandekwa** ujenzi umefikia 80%, **Makomero** ujenzi umefikia 95%. Igumila **80%, Kityelo** ujenzi umefikia 80%,
**Mhama mmoja** ujenzi umefikia 50%, **Maguguni** ujenzi umefikia 40% , **Igunga** ujenzi umefikia 80%.

**WKI. HWIG NA. 83/12/2021/2022 – UJENZI WA ICU NA NYUMBA ZA WATUMISHI**
Kaimu Mhandisi wa ujenzi aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao, alieleza Halmashauri ya wilaya ya Igunga imefanikiwa kupatiwa fedha ya ujenzi wa ICU kiasi cha Tshs 250,000,000 na ujenzi wa nyumba mbili za watumishi kiasi cha Tshs 180,000,000 ambapo moja itajengwa Mjini na nyingine itajengwa kijijini.
Aidha alieleza wasimamizi wa miradi hiyo walijengewa uwezo wa usimami wa miradi hiyo kupitia warsha ya siku mbili kuanzia tarehe 30 Desemba, 2021 hadi tarehe 01 Desemba, 2021 ilifanyika Mjini Dodoma.

**WKI. HWIG NA. 83/13/2021/2022 MPANGO WA KAZI KWA MRADI WA SEQUIP KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA.**
Kuna fedha zimeletwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za Sekondari jimbo la Manonga Kata ya Kitangiri Tshs 600,000,000 na Jimbo la Igunga Kata ya Mwamakona kiasi cha Tshs 600,000,000. Timu iliyoteuliwa ya kusimamia miradi ya ujenzi aliwasilisha mpango kazi wa ujenzi wa Sekondari ya Gulamali na Mwamakona.

Wajumbe walihoji fedha za ufuatiliaji zinatokana na fedha hizo hizo na je ujenzi utafanyika kwa mwaka mzima. Aidha walihojji kuhusu gharama za ufuatiliaji wa mradi huo uwepo.
Wajumbe walishauri majengo yaliyoainishwa Mhandisi wa ujenzi aandae BOQ ili wawe na pa kuanzia.

**WKI. HWIG NA. 83/14/2021/2022 – MENGINEYO**
Mbao na Madawati yaliyopo ndani ya eneo la Halmashauri yafanyiwe kazi yapelekwe sehemu husika kuepusha hoja. Maelezo yalitolewa kwamba Elimu Msingi nao wapo katika hatua ya kutengeneza Madawati kama bado mchakato ni mrefu mbao zihifadhiwe sehemu salama zisinyeshewe na mvua.

**WKI. HWIG NA. 82/15/2021/2022 - KUFUNGA KIKAO**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kikao kizuri. Kisha akafunga kikao saa 09:31 Alasiri

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| ........................ | ........................ |
| **TAREHE** 13/12/2021 | **TAREHE** 13/12/2021 |